**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI WA HOSPITALI YA WILAYA, ROMBO, KILIMANJARO

**18 JULAI, 2022**
**ROMBO**

- ***Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda (Mb.), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;***
- ***Mhe. Stephen Kagaigai, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro;***
- ***Mhe. Dkt.Godwin Mollel (Mb.), Naibu waziri wa Afya;***
- ***Waheshimiwa Naibu Mawaziri mliopo;***
- ***Ndg. Patrick Boysafi, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro;***
- ***Mhe. Stanslaus Nyongo (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii;***
- ***Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro;***
- ***Prof Abel N. Makubi, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya;***
- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;***
- ***Ndugu Willy Machumu, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro;***
- ***Mheshimiwa Col. Hamis M. Maiga, Mkuu wa Wilaya ya Rombo;***
- ***Viongozi wa Chama na Serikali wa Wilaya ya Rombo;***
- ***Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya;***
- ***Waheshimiwa Madiwani;***
- ***Viongozi wa vyama vya siasa mliopo;***
- ***Viongozi wetu wa Dini;***
- ***Watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Rombo;***
- ***Waandishi wa Habari;***
- ***Vikundi vya Burudani, Brass Band;***
- ***Mshereheshaji wa Viwango cya Kimataifa Peter Mavunde;***
- ***Wageni Waalikwa wote, Mabibi na Mabwana.***

***Rombo Oyee! Kilimanjaro Oyee!, Tanzania Oyee!***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….**

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupatia afya njema, kutusafirisha salama na kutuwezesha kufika hapa. Nawashukuru sana wanakilimanjaro kwa mapokezi mazuri tangu nilipowasili katika Mkoa huu. Kama mnavyofahamu, tangu Ijumaa nipo hapa Kilimanjaro kuzindua na kukagua

miradi ya afya pamoja na masuala mengine. Jumamosi, tulikuwa na tukio muhimu la kusherehekea miaka 96 tokea kuasisiwa kwa Hospitali ya Kibong'oto ambapo pia nilizindua Maabara ya kisasa kabisa katika Hospitali hiyo. Leo nimekuja hapa Rombo na kuweka jiwe la msingi wa Hospitali yetu kubwa ya Wilaya. Napenda nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na wananchi wote mliojumuika na sisi kwa ajili ya tukio hili. Kwa namna ya pekee, nawashukuru Viongozi wetu wa dini. Uwepo wenu na dua/sala umenibariki sana. Nimefurahi sana kwa upendo wenu mkubwa wananchi na kuwakuta mmekuja wengi sana, asanteni sana. Nawashukuru wote walioshiriki kusimamia vizuri ujenzi wa hospitali hii na Hongereni wana Rombo kwa kupata hospitali hii. Katibu Mkuu – Ardhi ameleta hapa hati ya kiwanja hiki ilipojengwa hospitali hii. Hati itunzwe. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wana Rombo na Wananchi wote wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kudumisha amani, utulivu, umoja na mshikamano na kwa kuendelea kuchapa kazi kulijenga Taifa letu mkishirikiana na Serikali yenu. **Hongereni sana!**

Salamu kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawapenda, amenituma nije Rombo, muendelee kutuunga mkono, tuwafanyie kazi.

Kituo cha kupoza umeme, hata yale mabango njiani nimesoma na nawaahidi changamoto ya umeme ninamwagiza Waziri aongeze kasi.

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Sekta ya afya inagusa maisha ya watanzania na ustawi wa maisha yetu. Upatikanaji wa huduma bora za afya ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora, ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za maendeleo ya nchi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imefanikiwa kuimarisha afya na ustawi wa Watanzania katika maeneo mbalimbali kwa kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinapatikana nchini kote na kwa makundi yote, hususan akina mama na watoto. Hali kadhalika, ujenzi wa mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ambapo inaelekeza Serikali kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma ya afya. Napenda niwapongeze sana Madaktari, Wauguzi na Watumishi wote wa afya hapa nchini. Tunategemea sana huduma yenu (utaalam, upendo, kazi ya mungu ya uponyaji). Mtunza majengo, tiba, dawa

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Nafahamu pamoja na juhudi hizi za Serikali katika kuboresha sekta ya afya, bado tuna changamoto zinazoendelea kuikabili sekta hii. Baadhi ya changamoto mmezitaja hapa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa madaktari bingwa, wauguzi,

wataalam wa huduma za kichunguzi, watoa dawa za usingizi na wataalam wa afya lishe pamoja na mazingira. Kama nilivyoeleza wakati wa Uzinduzi wa Maabara Mpya ya Afya ya Jamii katika Hospitali ya Kibong'oto, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya inaendelea kutatua changamoto hizi ili kuwapatia wananchi huduma wanayostahili. Vilevile, nimemwagiza Waziri wa Afya kujipanga na kuangalia namna ya kuziongezea watumishi pamoja na vifaa Hospitali zetu. Halikadhalika, ninaamini kwa ushirikiano na wadau wa sekta hii ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, tutaweza kupunguza na kutatua changamoto nyingi. Hivyo natoa rai kwa taasisi, mashirika na nchi rafiki, kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuboresha sekta hii ya afya. Naamini kwa dhati kabisa, tukishirikiana tunaweza kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya kuhakikisha afya njema na ustawi wa jamii yetu bila ya kumwacha mtu nyuma. Aidha, kuhusu changamoto ya uhaba wa nyumba za watumishi wa Hospitali, nawasisitiza TAMISEMI mjipange kujenga nyumba zaidi za watumishi.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa,***

Baada ya maelezo mazuri yaliyotolewa na Mawaziri, napenda nitumie fursa hii pia kutoa maelekezo yafuatayo:

**Jambo la Kwanza*,*** Hospitali hii ya Wilaya ambayo nimeweka jiwe la msingi, kama tunavyoona, baadhi ya majengo yamefikia hatua nzuri. Pamoja na kuwa huko nyuma kulikuwa na shida ya matumizi ya fedha, naelekeza TAMISEMI ifuatilie na kuhakikisha kwamba awamu ya 1 ya mradi huu unakamilika haraka mwezi Septemba 2022, vifaa tayari vimenunuliwa vije na Hospitali ianze kutumika ndani ya mwaka huu wa fedha kwa huduma zote muhimu. Tamisemi angezeni watumishi na nyumba. Lakini nafahamu pia Hospitali haifikiki kwa urahisi na wananchi wengi, hivyo naagiza Hospitali ya Kanisa ya Huruma ambayo ina hadhi ya Hospitali ya Wilaya, iendelee na hadhi hiyo. Na kwa nafasi hii natoa pongezi na shukrani kwa taasisi zote za dini zinazotoa huduma za afya hasa pale Serikali bado haijafika. Vilevile, nafahamu kuna barabara ya mpakani ya Holili-Rotimi-Tarakea yenye urefu wa takriban kilomita 53 inayopita karibu na Hospitali hii. Nafahamu kuwa fedha zimeshatengwa kwenye bajeti ya mwaka huu, hivyo naielekeza Wizara ya Ujenzi itangaze tenda na kuanza ujenzi wa barabara hii. TARURA nanyi muweke jicho barabara hii inayokuja hapa.

**Jambo la Pili**, Mheshimiwa Rais ni mama nafahamu Wilaya ya Rombo kuna shida ya maji na akina mama ndiyo wahanga wakuu. Lakini kuna mradi wa maji na Serikali imeshaleta shilingi bilioni 10 kwa ajili ya mradi huo hapa Rombo. Hivyo, naelekeza Wizara ya Maji Mhe. Naibu Waziri - Prisca unisikie ikamilishe haraka mradi huu ili kuwapatia wananchi wa Rombo maji ya uhakika. Na kwakuwa nipo katika Mkoa wa Kilimanjaro naomba nimkumbushe Waziri wa

Maji, ahakikishe mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe unakamilishwa haraka, wananchi wa maeneo hayo wamesubiri kwa muda mrefu.

**Jambo la Tatu**, taarifa aliyonipa Mkuu wa Mkoa imethibitisha kuwa Serikali ya awamu ya sita imeleta mabilioni ya fedha nyingi hapa Rombo na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na sekta ya afya. Na Serikali imefanya hivi kwa nchi nzima. Ninawataka watendaji wote wasimamie fedha hizi na kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa na thamani ya fedha inapatikana. Lakini pamoja na hili, naelekeza pia Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Halmashauri zote nchini ziweke nguvu katika kukusanya mapato ya ndani kwa ufanisi na kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na sio kukusanyia mifukoni.

**Jambo la Nne**, nimefurahishwa sana na ushirikiano mzuri uliopo baina ya viongozi wa CCM na viongozi wa Serikali katika Mkoa huu na wilaya zake. Wito wangu: muendelee kushikamana na kusimamia maendeleo ya kila Wilaya ikiwa pamoja na Wilaya hii ya Rombo, bila kusigana. Tunahitaji kasi zaidi katika kusimamia maendeleo ya Wilaya hii na Taifa kwa ujumla na hili litawezekana tu pale kila kiongozi anapowajibika ipasavyo katika nafasi yake. Hivyo, wasimamizi wote wa miradi hasa Wakurugenzi, Wahandisi, Waganga Wakuu wa Wilaya na Watendaji Wakuu wa idara nyingine, wahakikishe kasi yao inaendana na kasi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, wakuu hao wa Idara waweke kipaumbele cha bajeti kwenye miradi iliyoko kwenye Ilani ya CCM. Pia ninawaelekeza Mawaziri wote wanapotembelea Mikoa, wahakikishe wanatembelea Ofisi za CCM-Mkoa kupata uhalisia wa shughuli zinazofanyika katika Mikoa husika na kujua kero kubwa zinazowagusa wananchi.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa,***

**Jambo la Tano**, nimemsikia Mbunge wenu wa Rombo, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda akielezea juu ya eneo ambalo linapendekezwa kujengwa Chuo cha Wauguzi kitakachopokea wanafunzi kutoka hapa Rombo na Mikoa mingine ya nchi yetu. Kwa kuwa Warombo wametoa ardhi, naagiza Mawaziri wa Afya na TAMISEMI walifanyie kazi pendekezo hilo.

Wana Rombo nataka pia niwaeleze, mnabahati sana! Mmetuletea Mbunge mahiri na mwenye uwezo wa hali ya juu. Kwa kuwa ni mtoto wenu na ninajua kuwa nabii huwa hapati sifa akiwa kwao, lakini napenda niwaambie, Mbunge wenu ni Kazimoto kwelikweli! Mhe. Adolf Kazimoto Mkenda Oyee!! Aidha, nawapongeza Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ushirikiano wenu katika kutetea maslahi ya wananchi wenu. Vilevile, napenda kutumia nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mwenyekiti na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kwani imekuwa ikitupatia ushauri mzuri katika kuhakikisha Serikali inatoa huduma bora za afya kwa wananchi.

**Jambo la Sita**, sote tunafahamu kuwa mvua hazikuwa za kuridhisha katika mikoa mingi ya nchi yetu na hivyo ni muhimu kujiwekea tahadhari. Nazihimiza kaya zote kujiwekea akiba ya chakula. Na kwa upande wetu wa Serikali Kuu, Wizara ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) wameshapewa maelekezo ya kufuatilia na kufanya tathmini ya hali ya chakula nchini na kuhakikisha nchi ina akiba ya chakula ya kutosha.

Sambamba na hili la uhaba wa mvua naomba nigusie kuhusu Uharibifu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Shughuli zetu za kiuchumi, mathalani kilimo, zina uhusiano wa karibu na masuala ya mazingira. Hapa nchini hasa katika Mikoa ya kati na baadhi ya sehemu za Kanda za Juu Kusini, kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji, hasa ukichochewa na ukataji wa misitu hovyo kutokana na shughuli za kilimo na uchomaji mkaa. Hapa Rombo nimeelezwa kuwa katika maeneo ya msitu unaozunguka Mlima Kilimanjaro mnashirikiana vizuri na Serikali ya Mkoa na ya wilaya kutunza na kulinda mazingira.

Wana Rombo, natambua mnaelewa kuwa uharibifu wa mazingira unaleta changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kutotabirika kwa misimu ya mvua pamoja na ukame. Hivyo, naomba nitoe rai kwa wana Rombo na wananchi wote kwa ujumla, tuendelee kuwa macho na walinzi wazuri wa mazingira yetu. Tutunze misitu yetu ili tuweze kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi kwa manufaa ya kizazi hiki na kijacho. Tuyatunze mazingira ili na yenyewe yatutunze! Aidha, naelekeza watendaji wa Serikali katika ngazi zote, kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu ya mabadiliko ya tabianchi na mbinu bora za kilimo ambazo hazitasababisha uharibifu wa mazingira. Aidha, hakikisheni mnaendelea kusimamia sheria, kanuni, miongozo na taratibu ili kuepuka uharibifu wa mazingira na athari zake. Ninawapongeza kwa dhati wananchi na viongozi wa mkoa wa Kilimanjaro kwa utunzaji wa mazingira (miti, vyanzo vya maji) na kudumisha usafi wa makazi yenu. Kilimanjaro kwa sehemu kubwa ni safi na ya kijani**. Nawapongeza sana**.

***Ndugu Viongozi, Wananchi na Wageni Waalikwa,***

**Jambo la saba,** ambalo ningependa kuzungumza nanyi ni kuhusu Ulinzi na biashara kati yetu na majirani zetu wakenya. Nimeelezwa hapa hali ya biashara baina na wananchi wa hapa Rombo na nchi jirani inaendelea vizuri kutokana na mwenendo wa biashara kuimarika baada ya Janga la UVIKO-19. Lakini, ninawasihi wananchi mnapoendelea kufanya biashara, fanyeni kwa kufuata taratibu ikiwa ni pamoja na kupitia katika vituo rasmi vya mipaka na kujiepusha kufanya biashara kinyume cha sheria au kwa njia za magendo. Kupitisha biashara katika vituo rasmi vya mipaka mnasaidia Serikali yenu kupata kodi za uhakika ambazo zinaenda kutumika katika kuboresha huduma za kijamii kama ujenzi wa Hospitali hii na

miundombinu muhimu, kama barabara. Kama kuna vikwazo vinavyosababisha vijana wapitie njia za panya basi vijadiliwe na kutafutiwa ufumbuzi kupitia mabaraza ya biashara chini ya Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa.

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

Kwa mara nyingine tena napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Kamati za Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi wote kwa upendo wenu na maandalizi mazuri ya ziara yangu fupi mkoani Kilimanjaro lakini zaidi kwa kuendelea kudumisha amani na usalama ndani ya mkoa wetu na pia mpakani na nchi jirani ya Kenya. Napenda kutoa wito kwenu muendelee kuwa macho zaidi ili watu wetu waendelee kufanya shughuli za uzalishaji mali na biashara zaidi bila ya vikwazo au bughudha yoyote.

**Mwisho,** naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kuwakumbusha kuwa, nchi yetu itafanya Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23, Agosti 2022. Nawaomba wananchi wote wajitokeze kuhesabiwa na kutoa kila aina ya ushirikiano utakaohitajika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

**Mwenyezi Mungu Awabariki sana.**
**Asanteni kwa kunisikiliza!**